



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA MAJI USHIROMBO

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa mamlaka ya Maji)



WIZARA YA MAJI

**MKATABA WA MAKUBALIANO YA FUNDI KUFUNGA MFUMO WA UMEME CHANZO
CHA MAJI BULANGWA (PUMP HOUSE BULANGWA)**

MKATABA NA.LGA.113/2022/2023/MJ/03

MKATATABA WA FUNDI KUFUNGA MFUMO WA UMEME

KATI YA

NA

MWAJIRI:

**MKURUGENZI WA MAMALAKA YA MAJI,
MJI WA USHIROMBO**

SLP 02

BUKOMBE

MWAJIRIWA:

**SILVANUS WILSON MAGARE
SLP 02**

USHIROMBO

24/08/2022

**MKATABA WA MAKUBALIANO YA FUNDI KUFUNGA MFUMO WA
UMEME CHANZO CHA MAJI BULANGWA (PUMP HOUSE BULANGWA)
KATI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA USHIROMBO (UWSSA)
NA SILVANUS WILSON MAGARE (FUNDI UMEME)**

**MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA USHIROMBO (UWSSA) SLP 02
BUKOMBE** (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama “**mwajiri**”) kwa upande
mmoja,

NA

SILVANUS WILSON MAGARE (FUNDI UMEME), WA SLP 02 USHIROMBO (ambaye
katika mkataba huu atajulikana kama “**mwajiriwa**”) kwa upande mwingine.

KWA KUWA: Mwajiri anayo kazi ambayo amehiyari na anayo nia ifanywe na
mwajiriwa, kazi ya kufunga mfumo wa umeme Bulangwa pump house.

NA KWA KUWA: Mwajiriwa yuko tayari na anao uwezo wa kufunga mfumo wa
umeme.

HIVYO BASI MKATABA huu ni ushuhuda wa makubaliano **kwamba**:

Makubaliano haya yanafanyika leo hii tarehe. ~~24~~...mwezi....~~08~~.....mwaka...~~2022~~...

1. Mwajiriwa anao uwezo wa kufanya kazi ya kufunga mfumo wa umeme na
kazi hiyo atatakiwa kuifanya kwa kuzingatia viwango na ubora unaotakiwa,
na hili litakuwa sharti la msingi la mkataba huu
2. Msimamizi wa kazi hii ni Mhandisi wa maji RUWASA Bukombe ambaye
atatoa maelekezo ya kazi, atasimamia, atakagua na kutoa taarifa ya ubora wa
kazi kwa mwajiri.
3. Mwajiri atapaswa kumlipa Mwajiriwa kiasi cha Tsh.....150,000/-....

4. Kwamba mwajiriwa atafanya kazi ya kufunga mfumo wa umeme kwa kuzingatia “specifications” na ‘BOQ’ ambavyo atakabidhiwa na msimamizi wa kazi na nyaraka hizi zitaambatanishwa na kuwa sehemu ya makubaliano haya
5. Endapo kutatokea mgogoro wa aina yoyote kati ya mwajiri na mwajiriwa, mgogoro huo utatatuliwa kwa njia ya usuluhishi utakao simamiwa na Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe na endapo usuluhishi utashindwa kufikia muafaka, basi mgogoro huo utaelekezwa katika vyombo vyaa sheria (mahakama) na maamuzi yatakayotolewa na mahakama yatakuwa ya mwisho.
6. Endapo kutakuwa na malalamiko ya aina yoyote kutoka kwa mwajiriwa, yatawasilishwa kwa njia ya maandishi kwenda kwa mwajiri, na yatawasilishwa ndani ya siku mbili baada ya mgogoro kutokea.
7. Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku za kwenye kalenda bila kuondoa siku za sikukuu na mapumziko, kuanzia tarehe 24.08.2022 hadi tarehe 29.08.2022
8. Mkataba huu unaweza kusitishwa na upande wowote wa mkataba kwa kutoa taarifa ya siku saba (7) kwa maandishi inayoeleza sababu za msingi za kusitisha mkataba huu.

Pande zote mbili zimekubaliana na kutiliana saini kwenye makubaliano haya na ni wazi kuwa kila upande umesoma na kuelewa vipengele vyote vyaa mkataba huu, na unatiwa saini leo tarehe 24.....mwezi.....08.....2022.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji,
 Jina kamili..... *Getruda Dang'kuus*
 Saini.....
 Tarehe..... *24/08/2022*
 Mhuri wa ofisi..... *MANILAKA YA MAJI SAFI NA USAFI
 WA MAZIWA KU BUKOMBE
 STATION 12
 BUKOMBE*

Umesainiwa na kupokelewa(mwajiriwa)
 Jina Kamili *SILVANUS KI MAGARE*
 Saini.....
 Tarehe..... *24/08/2022*
 Wadhifa *FUNDI MUSONAMIZI*

Mwenyekiti wa Bodi wa mamlaka ya maji
 Jina kamili *LAMEEZA WARANGA*
 Saini.....
 Tarehe..... *24/08/2022*
 Mhuri wa ofisi.....

Shuhuda wa mwajiriwa
 Jina Kamili *MUSA BO THOMAS*
 Saini.....
 Tarehe..... *24/08/2022*
 Wadhifa *FUNDI MUSONAMIZI*

MHURI WA MWANA SHERIA WA HALMASHAURI.
 JINA KAMILI *JOSEPH N. KOMBA*
 CHEO *CLO* SAHIHI *K. Komba*
 TAREHE *24/08/2022*

